

Namna nzuri ya kuhudumia nywele zako za asili kirahisi

By SW - Melkisedeck Shine · April 18, 2022

Dondoo za Urembo na Mitindo · #Karibu AckySHINE · #SMS, Vichekesho, Mahusiano, Biashara na Ujasiriamali, Afya, Chemsha Bongo, Dini pamoja na Vitabu kwenye PDF

Kwa wale ambao tuna nywele asilia (natural hair), tayari tunafahamu changamoto kadhaa tunazokumbana nazo. Kwa wale mnaofikiria kuanza kuwa na nywele asilia, karibuni sana tuendeleo kujuzana namna ya kutunza nywele zetu kama tulivyopewa na Mungu.

Katika mada ya leo, nitakwenda kuzungumzia vitu vya kuzingatia ili kuikuza nywele yako asilia kwa haraka zaidi. Je, unazifahamu nywele zako vizuri? Una nywele za aina gani? Zina tabia gani? Zinataka nini?

Zifuatazo ndizo njia ya kuzihudumia nywele zako; 1. Kuzikubali kama zilivyo na kuzipenda.

Yani hapa ndo shule ilipolalia kabisaa maana ukizijua tu basi utazihudumia kwa usahihi. Unatakiwa kuangalia namna gani nywele zako zinanyonya unyevu. Unajuaje?

Chukua kikombe, kijaze maji safi. Ukipata glass itakuwa vizuri zaidi.

Chomoa unywele mmoja kichwani, hakikisha unatoka na kale kamzizi kake keupe keupe hivi.

Tumbukiza unywele wako kwenye glass yako ya maji hakikisha imeingia yote. Kama ikizama hapo hapo na hainyanyuki tena, basi nywele zako zinanyonya unyevu kwa haraka kabisa. Kama inachukua muda kuzama, au haizami kabisa, nywele zako zinanyonya unyevu taratibu au zinanyonya kwa shida.

Mbadala, unaweza baada ya kuosha suuza na maji ya vuguvugu halafu weka mafuta ya kimiminika. Inasaidia sana.

Mimi nina aina gani?.. Nina nywele zinazonyonya unyevu haraka. 5. Mafuta ya Kupaka kichwani.

Ni ya muhimu mnoo!. Nimefanya utafiti wa kina nimeona mafuta ya nazi yanaweka afya nzuri kwa nywele aina nyingi hivyo na mimi nikaanza kuyatumia. Kwangu mimi, mafuta ya nazi ya kutengeneza mwenyewe yamenikubali sana. Japo huwa nanunua pia mafuta kama ya olive (extra virgin) na ya tea tree. 6. Kuzichambua vizuri kabla ya kuchana.

Uwe mkarimu na mwenye subira kwa nywele zako. Mimi zikijifunga huwa nazichambua kwa mikono taratibu wakati mwingine nazilowesha na maji kwa mbali halafu nachana kwa chano lenye mapana sio ambalo reli zake zimebanana. Sio kitana. Chano kubwa (wide

toothed comb). 7. Usizisumbue mara kwa mara na usuke mitindo ya kuzitunza zikue.

Kama unataka zikue haraka, usizisumbue sana. Unaweza ukasuka mitindo mizuri tu ukakaa nazo wiki nzima au kadri zitakavyodumu. Au upunguze kuzichana mara kwa mara lakini utafute siku kama wikiendi ukae uzichambue taratibu na vidole kuondoa mafundo. Kuchana mara kwa mara zinapukutika, zinaanguka. Zitakua lakini sio kwa kasi ya kama ukizisuka ukaziacha kwa muda. 8. Punguza matumizi ya vitu vya moto kwenye nywele zako kama pasi ya nywele na vingine vya hivyo.

Mimi dryer la nywele situmii zaidi ya mara mbili kwa mwezi. Mara nyingi naziacha zikauke na hewa hata kama nimezifunga rollers natoa kesho baada ya masaa 24